UQAB
Jarida la
TOLEO MAALUM
Toleo 39- Shaban 1441 H / Aprili 2020 M

# NI WAKATI WA KHILAFAH

“Hii kumbukumbu ya tisini na tisa iwe ndio utangulizi wa ushindi mkubwakabla kumbukumbu ya mia moja ya kuvunjwa Khilafah”





بسم الله الرحمن الرحيم

# Hotuba ya Amiri wa Hizb ut Tahrir, Mwanachuoni Mkubwa, Ata Bin Khalil Abu Al-Rashtah

# Kuhusiana na Tukio la Kumbukumbu ya 99 ya Kuvunjwa Dola ya Khilafah

(Imetafsiriwa)

Sifa njema zote ni kwa Mwenyezi Mungu, na swala na salamu zimshukie Mtume wa Mwenyezi Mungu, jamaa zake na maswahaba zake, na wafuasi wake …

Kwa Ummah wa Kiislamu kwa jumla, umma bora uliotolewa kwa wanadamu… na kwa Mashababu wa Hizb ut Tahrir haswa, ambao Mwenyezi Mungu amewakirimu kwa ubebaji Ulinganizi Wake kwa ikhlasi na imani… **na kwa wageni wa tovuti, wanaozuru kutokana na mapenzi ya kheri na nuru inayobeba kwa wote: Assalamu Alaikum Wa Rahmatullah Wa Barakatuh**

Katika siku hii, miaka tisini na tisa iliyopita, mhalifu wa zama hizi Mustafa Kamal aliivunja Khilafah, na ingawa hili lilikuwa peupe hadharani, na kunakiliwa kwa dalili, bali kwa dalili zaidi ya moja, kuwa huu ni ukafiri wazi wa kufutilia mbali utawala wa Uislamu, na kwamba watekelezaji uhalifu huu wanastahili kupigwa vita kwa upanga kwa mujibu wa Hadith ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw), iliyo simuliwa na Bukhari na Muslim kutoka kwa Junada ibn Abi Umaiya aliyesema:

Tuliingia kwa 'Ubada bin As-Samit hali ya kuwa yeye ni mgonjwa. Tukasema, "Mwenyezi Mungu akupe afya. Je, hutuelezi na sisi Hadith uliyoisikia kutoka kwa Mtume (saw) na ambayo kwayo Mwenyez Mungu huenda akakunufaisha?" Akasema, "Mtume (saw) alituita na tukampa Ahadi ya Utiifu kwa Uislamu, na miongoni mwa masharti ambayo kwayo alichukua Ahadi hiyo kwetu, بَايَعَنَا عَلَى

**السَّمْعِ وَالطَّاعَةِ فِي مَنْشَطِنَا وَمَكْرَهِنَا وَعُسْرِنَا وَيُسْرِنَا وَأَثَرَةً عَلَيْنَا وَأَنْ لَا نُنَازِعَ الْأَمْرَ أَهْلَهُ إِلَّا أَنْ تَرَوْا كُفْراً بَوَاحاً عِنْدَكُمْ مِنْ اللَّهِ فِيهِ بُرْهَانٌ» "ilikuwa ni kwamba tutasikiza na kutii (maamrisho) kwa tunayo yapenda na tunayo yachukia na mazito kwetu na mepesi kwetu na kumtii kiongozi na kumpa haki yake hata kama yeye hatatupa haki yetu, na tusizozane naye isipokuwa tukiuona ukafiri ulio wazi ambao tunao uthibitisho kutoka kwa Mwenyezi Mungu."**

Jukumu lilikuwa ni kupigana naye na kujitolea muhanga kwa hili kwa gharama yoyote ile, namna itakavyokuwa kubwa. Lakini dhalimu huyu Ummah hawakumkabili kwa anayostahiki, kummaliza! Hivyo basi historia ya Ummah ikaingia giza, Ummah ambao ni bora uliotolewa kwa wanadamu uliokuwa na Dola moja ya Khilafah, uliokuwa ukiogopewa, na kubeba Haki na uadilifu, sasa umekuwa ni mipasuko zaidi ya hamsini, ukiwa umegawanyika miongoni mwao, umeshindwa nguvu na wale wasiokuwa na huruma juu yao, na kupuuzwa mambo yao. Na sio hili tu, bali wanatawaliwa na watawala Ruwaybidha (wajinga) ambao ni watiifu, wanajisalimisha kwa makafiri, na wafuasi wa wakoloni, utajiri wao ndio unaopeleka uchumi wa maadui hawa wa Dini ya Mwenyezi Mungu. Ama uchumi wa nchi na watu wao, umezorota na kufujwa, watu wake hawanufaiki nao, bali hali yao inaeleza yote (kama vile mifugo walio jangwani wanaokufa kwa kiu ilhali maji (mzigo) yamebebwa migongoni mwao). Hili linafanyika machoni na masikioni mwa watawala Ruwaybidha (wajinga) hawa. Umasikini umeenea miongoni mwa watu, isipokuwa kwa pote la watawala na wapambe wao, ambao hupata zawadi iliyofinikwa kwa fedheha na aibu kwa huduma yao kwa mabwana zao wakoloni, khiyana kwa Mwenyezi Mungu na Mtume Wake na waumini, na kizuizi katika njia ya Mwenyezi Mungu Al-Aziz Al-Hakim.

**Enyi Waislamu,** Khilafah ndio kadhia nyeti ya Waislamu, ambayo kwayo Hudud (mipaka) huchungwa, heshima huhifadhiwa, ardhi hukombolewa, na Uislamu na Waislamu hutukuzwa, na yote haya yameandikwa katika Kitabu cha Al-Aziz Al-Hakim, na Sunnah ya Mtume Wake (saw), na Ijma' ya Maswahaba zake, Mwenyezi Mungu awe radhi nao. Inatosheleza kwa Muislamu kuyasoma mambo matatu yafuatayo ili kutambua ni jinsi gani Khilafah ni faradhi nzito na kubwa iliyoje; nayo ni haya yafuatayo:

**Kwanza**: Maneno yake, swala za Mwenyezi Mungu na salamu zimshukie yeye, yaliyo simuliwa na At-Tabarani katika Al-Ma'jam Al-Kabeer kutoka kwa Asim, kutoka kwa Abu Saleh, kutoka kwa Muawiyah, aliyesema: Nilimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw), akisema:

**«مَنْ مَاتَ وَلَيْسَ فِي عُنُقِهِ بَيْعَةٌ مَاتَ مَيْتَةً جَاهِلِيَّةً» "Yeyote anaye kufa na hana shingoni mwake ahadi ya utiifu (kwa mtawala) amekufa kifo cha kijahiliya."**

Hii ni dalili ya ukubwa wa dhambi kwa Muislamu aliye na uwezo kutofanya kazi ya kumsimamisha Khalifah ambaye atampa bay'ah iliyo shingoni mwake, yaani ni dalili ya kumtafuta Khalifah anayestahiki bay'ah iliyo shingoni mwa kila Muislamu kupitia uwepo wake.

**Pili:** Lilikuwa ni jambo lililo washughulisha Maswahaba wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) la kusimamisha Khilafah na kumpa bay'ah Khalifah kabla ya kushughulika kwao na mazishi ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw). Ingawa, kuharakisha mazishi ni jambo lililo hitajika na Shariah. Imeelezwa katika Ma'rifat Al-Sunan Wal Athar cha al-Bayhaqi: "Ash-Shafi'i amesema katika riwaya ya Abi Saeed: Inafadhilishwa zaidi kuharakisha kumzika maiti, endapo kifo kitathibitishwa." Hii ni kwa maiti yeyote, vipi basi ikiwa maiti huyu ni Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw), licha ya hayo Maswahaba walifadhilisha kutoa bay'ah kwa Khalifah kuliko kumzika Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw), na hivyo basi kuthibitishwa kwa Ijma'a ya Maswahaba kumsimamisha Khalifah kwa kuchelewesha kwao kumzika Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) baada ya kufa kwake na kushugulika kwao na uteuzi wa Khalifah.

**Tatu:** Umar, Mwenyezi Mungu awe radhi naye, siku ya kifo chake, alikuwa ameweka muda maalumu wa kumchagua khalifah kutoka miongoni mwa sita (Maswahaba) walio ahidiwa Pepo, usiozidi siku tatu … Kisha akaagiza kuwa endapo Khalifah hatachaguliwa (hawataafikiana) katika siku tatu, wale watakaokuwa hawaafikiani watauawa baada ya siku tatu hizo. Na akawapa jukumu hilo watu hamsini miongoni mwa Waislamu kutekeleza hili, yaani kumuua yule asiyekubali, ingawa walikuwa wameahidiwa Pepo, na walikuwa katika watu wa Shura, na walikuwa katika Maswahaba wakubwa. Hili lilifanyika machoni na masikioni mwa Maswahaba, hakuna riwaya yoyote kuwa yeyote kati yao hakuafiki au alikataa hili. Hivyo basi ni Ijma'a ya Maswahaba kuwa ni haramu kwa Waislamu kubakia bila ya Khalifah kwa zaidi ya michana mitatu pamoja na usiku wake, na ni "mafungu mangapi ya siku tatu" yapetupitia, *La Hawla Wa La Quwata Ila Billah*! Hivyo basi Khilafah, Enyi Waislamu, ni kadhia muhimu na nyeti kwa Waislamu na ni kadhia iliyoje hii!

**Enyi Waislamu,** licha ya hili, hatukati tamaa na rehma ya Mwenyezi Mungu, ﴿إِنَّهُ لَا يَيْأَسُ مِنْ رَوْحِ اللَّهِ إِلَّا الْقَوْمُ الْكَافِرُونَ﴾ **"Hakika hawakati tamaa na faraji ya Mwenyezi Mungu isipokuwa watu makafiri."** [Yusuf: 87]

Hususan kwa kuwa Mwenyezi Mungu (swt) amewaahidi wale walio amini na kutenda mema kuwa atawafanya makhalifa (watawala) katika ardhi ﴿وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنْكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ﴾ **"Mwenyezi Mungu amewaahidi wale walio amini miongoni mwenu na wakatenda mema, ya kwamba atawafanya makhalifa katika ardhi kama alivyo wafanya makhalifa wa kabla yao"** [An-Nur: 55].

Vilevile, Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) alitoa bishara njema ya kurudi kwa Khilafah kwa njia ya Utume baada ya utawala wa kidhalimu ambao tunaishi chini yake. «ثُمَّ تَكُونُ خِلَافَةً عَلَى مِنْهَاجِ النُّبُوَّةِ» **"Kisha kutakuwa na Khilafah kwa njia ya Utume."** [Imesimuliwa na Ahmad kutoka kwa Hudhayfah ibn al-Yaman, Mwenyezi Mungu awe radhi naye].

Lakini, tunathibitisha na kurudia yale tuliyo tangulia kusema, kuwa Mwenyezi Mungu Al-Qawi Al-Aziz atatunusuru ikiwa tutamnusuru, kupitia kuwa miongoni mwa wafanyi kazi wenye ikhlasi waaminifu. Ni Sunnah ya Mwenyezi Mungu kuwa malaika hawata teremshwa kufanya kazi kwa niaba yetu na kusimamisha Khilafah kwa ajili yetu, huku tukiwa tumeketi na kubarizi makochini mwetu! Bali, Mwenyezi Mungu (swt) huwateremsha malaika, kwa idhini ya Mwenyezi Mungu, kutusaidia huku tukiwa tunafanya kazi, na hiyo ndiyo ahadi ya Mwenyezi Mungu katika kila ushindi, ima iwe ni katika kusimamisha Khilafah kwa kazi ya kheri na kuimakinisha, au iwe ni katika ufunguzi na ushindi wa Mwenyezi Mungu kupitia kupigana katika njia yake (swt).

Tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuukirimu Ummah huu kwa kuasisiwa Hizb ut Tahrir, inayojitolea kwa kazi makinifu na ya ikhlasi, kwa idhini ya Mwenyezi Mungu, kurejesha maisha kamili ya Kiislamu kupitia kusimamisha Khilafah ya Uongofu. Ni kiongozi ambaye hawadanganyi watu wake. Ni chama ambacho kheri yake inang'aa, na wote ambao hawawezi kuhimili kheri hii wanaporomoka kutokana nayo. Hii ndiyo tunayo amini kuwa ndiyo hali na tunaamini kuwa mashababu (wanachama) wake wanaofanya kazi nayo wako makini na wenye bidii, wafanyakazi watiifu, kwa idhini ya Mwenyezi Mungu, walio na hamu ya Akhera juu ya matarajio yao ya duniani. Na wanafanya kazi mchana na usiku, wakitaraji kupata Rehma za Mwenyezi Mungu; kuwa ahadi

Yake (swt) na bishara njema ya Mtume Wake (saw) zitatimia kupitia mikono yao, na hili ni sahali kutimizwa na Mwenyezi Mungu.

**Kwa kutamatisha,** faradhi ya kusimamisha Khilafah, Enyi Waislamu, haiko tu juu ya wanachama wa chama hiki pekee, bali pia juu ya kila Muislamu mwenye uwezo, kwa hiyo tupeni nusra, Enyi Waislamu, na tupeni nusra Enyi majeshi ya Waislamu, na rejesheni izza ya Answar (walionusuru) walipoinusuru Dini ya Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu aliwafanya kuwa sawa na Muhajirina, akawasifu na akawa radhi nao katika Kitabu Chake Kitukufu bila ya mipaka. Mbali na hayo kazi hii imefungika kwa wafuasi wake kwa wema (Ihsan).﴿ **وَالسَّابِقُونَ الْأَوَّلُونَ مِنَ الْمُهَاجِرِينَ وَالْأَنْصَارِ وَالَّذِينَ اتَّبَعُوهُمْ بِإِحْسَانٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمْ وَرَضُوا عَنْهُ وَأَعَدَّ لَهُمْ جَنَّاتٍ تَجْرِي تَحْتَهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا أَبَداً ذَلِكَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ**﴾ **“Na wale wali tangulia, wa kwanza, katika Wahajiri na Ansari, na walio wafuata kwa wema, Mwenyezi Mungu ameridhika nao, na wao wameridhika naye; na amewaandalia Bustani zipitazo mito kati yake, wadumu humo milele. Huko ndiko kufuzu kukubwa.”** [At-Taubah: 100]

Hii ni kwa sababu ya thamani, malipo makubwa, na utukufu wa kuheshimika ambao kazi ya kunusuru Dini ya Mwenyezi Mungu na kusimamisha Khilafah iliyo nayo, kufikia hadi malaika kubeba mwili wa Saad bin Muadh, Sayyid al-Answar (Bwana wa Maanswar), Mwenyezi Mungu awe radhi naye, kama ilivyo elezwa katika Al-Mustadrak juu ya Al-Sahihain na Al-Hakim kuhusu utukufu wa kitendo cha kuinusuru Dini ya Mwenyezi Mungu.

**Mwisho kabisa,** yeyote atakaye inusuru kazi hii ya kusimamisha Khilafah kabla ya kusimama kwake, malipo yake ni mengi na makubwa kuliko kuinusuru Khilafah baada ya kusimama kwake ﴿ **لَا يَسْتَوِي مِنْكُمْ مَنْ أَنْفَقَ مِنْ قَبْلِ الْفَتْحِ وَقَاتَلَ أُولَئِكَ أَعْظَمُ دَرَجَةً مِنَ الَّذِينَ أَنْفَقُوا مِنْ بَعْدُ وَقَاتَلُوا وَكُلّاً وَعَدَ اللَّهُ الْحُسْنَى وَاللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ خَبِيرٌ**﴾ **“Hawawi sawa miongoni mwenu wenye kutoa kabla ya Ushindi na wakapigana vita. Hao wana daraja kubwa zaidi kuliko wale ambao walio toa baadae na wakapigana. Na wote hao Mwenyezi Mungu amewaahidia wema. Na Mwenyezi Mungu anazo khabari za mnayo yatenda.”** [Al-Hadid: 10].

Na tunamuomba Mwenyezi Mungu (swt) kwa dhati kuwa kumbukumbu hii ya tisini na tisa iwe ndio utangulizi wa ushindi mkubwa wa Mwenyezi Mungu kabla ya kumbukumbu ya mia moja ya kuvunjwa Khilafah na kisha Khilafah ya Uongofu itang'aa tena ulimwenguni.


﴿وَيَوْمَئِذٍ يَفْرَحُ الْمُؤْمِنُونَ * بِنَصْرِ اللَّهِ يَنْصُرُ مَنْ يَشَاءُ وَهُوَ الْعَزِيزُ الرَّحِيمُ﴾

**"Na siku hiyo Waumini watafurahi * Kwa nusura ya Mwenyezi Mungu humnusuru amtakaye. Naye ndiye Mwenye nguvu Mwenye kurehemu."** [Ar-Rum: 4-5]

**Wa Assalamu Alaikum Wa Rahmatullah Wa Barakatuh**
**Ndugu yenu,**
**Ata Bin Khalil Abu Al-Rashtah**
**Amiri wa Hizb ut Tahrir**

Jumatatu, 28 Rajab 1441 H 23/3/2020 M

# Katika Makumbusho ya Miaka Tisini na Tisa ya Kuvunjwa kwa Khilafah, Isimamisheni Kabla ya Kutimia Miaka 100 (Imetafsiriwa)


THE CALIPH DEPOSED.

SCENE IN THRONE ROOM.

EXPULSION AT NIGHT.

(FROM OUR OWN CORRESPONDENT.)

CONSTANTINOPLE, MARCH 4.

The Caliph Abdul Mejid, his son Prince Omar Farukh Effendi, and the members of his immediate family were compelled to leave Constantinople during the night.

Miaka tisini na tisa ... Huu hapa mwaka mwingine umepita katika maisha yetu, na kumbukumbu ya kuvunjwa kwa Khilafah imerudi kutuzuru tena, kutukumbusha kuwa Ummah wa Kiislamu umechelewa kutoa ahadi ya utiifu kwa Imamu kwa miaka yote hiyo! Kwa hiyo, je, itasimamishwa leo kabla ya ukumbusho wa mwaka wa 100?!

Miaka tisini na tisa ... Na suala la kupoteza "utukufu na hadhi" miongoni mwa mataifa ni suala ambalo damu huchemka katika mishipa ya Ummah wa Kiislamu ... ambapo watu wake wametoka katika mapinduzi ya kihistoria yasio ya kawaida, na zile zilizozingatiwa kuwa “tawala zisizo yumbishwa” zilipinduliwa. Kwa hiyo, je, itasimamishwa leo kabla ya maadhimisho ya mwaka wa 100?!

Miaka tisini na tisa ... Na kafiri mkoloni Mmagharibi aidhinisha mipango, asimamia njama, na kutafuta kuzibadilisha upya njia zake na namna zake za kuuweka Ummah wa Kiislamu katika hali ya kutawanyika bila ya serikali na dhaifu bila nguvu. Kwa hiyo, je, itasimamishwa leo kabla ya maadhimisho ya mwaka wa 100?!




Bado tunaiona Khilafah ikitajwa wakati wote katika mizunguko, miongoni mwa watu, katika wanaoichukia, kati ya familia, katika vipindi na makala. Khilafah imekuwa maoni ya umma miongoni mwa Waislamu, wote ambao wameshangazwa kwa jinsi itakavyorudi! Kila mmoja anafahamu utukufu wake wakati itakaporudi, na kila mmoja anajua kuwa wakati itakaporudi itazindua nguvu za Ummah na kuregesha kutekeleza jukumu lake katika ulimwengu, kuwa muokozi wa ulimwengu huu kutoka katika hali iliyofikia. Vipi hatuwezi kutambua utukufu wa Khilafah, kwani ni serikali ambayo idadi ya watu wake imezidi bilioni moja na nusu wanaotamani kurudi kwake karibuni. Waislamu bilioni moja na nusu, wanaume na wanawake wanaozingatia kila mmoja wao kama kaka na dada kutoka familia moja inayofunika ulimwengu. Mwenyezi Mungu (swt) anasema: ( إِنَّمَا الْمُؤْمِنُونَ إِخْوَةٌ) “Hakika Waumini ni ndugu” [Al-Hujurat: 10]

Utukufu wa Ummah wa Kiislamu umefungika kwa masharti matatu kwa utukufu wa mataifa, ambayo ni, "Ummah, Itikadi na Dola." Ama kuhusu Ummah, upo, umejaa nguvu na imara, ambapo unajaza viwanja vya mji kwa vijana wa kiume na wa kike. Ama kuhusu Itikadi, pia ipo. Ambapo ufahamu wa maelezo yake na utafiti wa matumizi yake umefanywa na wale ambao wanaujali sana Uislamu, wakiongozwa na Hizb ut Tahrir, ambao wameandaa kurudi kwa Khilafah kama "dola ya Khilafah iliyoendelea" na wameandaa sheria halali ya nidhamu ya kisiasa iliyopitishwa na vyanzo vya sheria za Kiislamu.

Ama kuhusu Dola, inajumuisha nguvu. Kwani dola huchukua nguvu zilizotawanyika za watu na kuwakusanya wao katika kiganja kimoja, hupanga

uwezo wao uliotawanyika, kuwafanya wao kuwa nguvu yenye natija. Kwa Ummah wa Kiislamu, dola ni kama kinywaji cha kushangaza na dawa ya ajabu. Kwa kuwepo kwa dola ya Kiislamu, nguvu za Ummah zitapangiliwa, na italipua nguvu zake, na kwa kukosekana kwake huanguka na rasIlimali zake kuporwa. Ndio maana lazima tutambue kuwa kuungana kwa Ummah wa Kiislamu na dola yake itakuwa ni tukio sawia na dhoruba ya nyuklia katika historia ya binadamu. Itayafundisha mataifa jinsi ya kushughulikia mlipuko wa magonjwa na maradhi, na itawakomesha wanaoabudu ng'ombe wa India kutokana kufikiria kuhusu minong'ono ya shetani, na itawafanya wao kuonja matokeo ya vitendo vyao.

Na kwa hili, kwa jina la Mwenyezi Mungu na juu ya baraka za Mwenyezi Mungu, katika ukumbusho wa 99 wa kuvunjwa kwa Khilafah, tunazindua kampeni pana ya kiulimwengu ambayo tunawalingania Ummah wa Kiislamu na watu wake, wanachuoni, majeshi, na watu wenye nguvu kuharakisha kusimamishwa kwa Khilafah kabla hatujafika mwaka wa mia moja! Ili tupate radhi za Mwenyezi Mungu (swt) na ili historia iweze kurekodi kuwa sisi ni Ummah muhimu ambao uliweza kurudi ulimwenguni chini ya miaka mia moja.

Katika tukio hili, kutakuwa na hotuba yenye maana kubwa na Amiri wa Hizb ut Tahrir, mwanachuoni mkubwa Ata Bin Khalil Abu Al-Rashtah, Mwenyezi Mungu amlinde, katika tukio la ukumbusho wa 99 wa kuvunjwa kwa dola ya Khilafah katika tangazo maalumu kwenye kituo cha Runinga ya Al-Waqiyah baada ya Maghrib, Jumapili, ambayo itakuwa ni usiku wa Jumatatu, 28 mwezi mtukufu wa Rajab 1441 H sawia na 23/3/2020 M.

Imepokewa kutoka kwa Ubay ibn Ka'b, radhi za Mwenyezi mungu ziwe naye, alisema: Mtume wa Mwenyezi Mungu, rehma na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na familia yake, alisema

**«بَشِّرْ أُمَّتِي بِالسَّنَاءِ وَالرِّفْعَةِ وَالتَّمْكِينِ فِي الْبِلَادِ...»**

“Wabashirie Ummah wangu ushindi, umaarufu na umakinifu katika ardhi...”




# fikra ilio wadia wakati wake


Katika mwezi huu wa Rajab, 1441, itatimia miaka 99 tokea kuvunjwa kwa Khilafah kupitia ushirikiano wa wasaliti miongoni mwa Waarabu na Waturuki pamoja na maadui wakoloni. Katika Ulimwengu wote wa Waislamu, kukosekana kwa utekelezaji wa hukmu zote za Mwenyezi Mungu kunahisiwa, kunakotupelekea kukata tamaa. Pakistan haina tofauti, kwani matumaini ya mwisho ya nidhamu ya utawala nchini Pakistan imetuvunja moyo na kuvunjwa vipande vipande. Bila shaka, serikali ya "mabadiliko" imeshindwa kuzuia ufisadi, kuharibiwa uchumi wetu na kuteketezwa usalama wetu na wakoloni hivi leo.

Tumekata tamaa kwani ufisadi umepata maisha mapya, kukiwa hakuna pesa iliyorudishwa kutoka kwenye safu ya majenerali na wanasiasa mafisadi, waliojaza matumbo yao kwa fedha zetu na kukaribia kupasuka. Tumekata tamaa kwa kuwa Pakistan imezamishwa hadi shingoni ndani ya madeni, yaliyo na riba inayochukiza, ambayo ni wito wa vita kutoka kwa Mwenyezi Mungu (swt) na Mtume wake (saw). Tumechanganyikiwa kutokana na masharti ya kikoloni kuhusiana na mikopo ya kigeni inayo nyonya rasilimali zetu, huku ikitoa kipigo kwa viwanda vyetu vya ndani, kilimo na sarafu kuifikisha kwenye kiwango kisichostahiki ili kudumisha ubabe wa uchumi wa kigeni.

Tunatikisa vichwa vyetu kwa huzuni wakati vilio vya Waislamu wa Kashmir iliyotawaliwa vikikumbana na "kizuizi", kauli zisizo na meno na hatua za ishara tu, sambamba na sera ya Amerika kuruhusu kuibuka Dola ya Kihindu kama ni Akhund Bharat, "India Kuu". Na tumekuwa wenye wasiwasi huku utawala unaangusha nyundo juu ya miguu yetu, kwa kuwa kama wasaidiaji tulioajiriwa kuhifadhi uwepo wa "Raymond Davis" mwanakandarasi binafsi wa Amerika wa masuala ya kijeshi nchini Afghanistan, wakikaribia vifaa vyetu vya nyuklia, chini ya kisingizio cha mpango unaopigiwa tarumbeta wa uondoaji mchache wa vikosi vya kijeshi vya kawaida.

Hakuna mwisho wa kukata tamaa kwetu, isipokuwa tuangalie mbele zaidi ya nidhamu iliyobuniwa na wanadamu kuelekea Dini yetu Tukufu, iliyofunuliwa na

Bwana wa Ulimwengu, Mwenyezi Mungu (swt). Tumeshuhudia namna gani mtu mmoja, aliyeungwa mkono na jeshi letu, hawezi kuchukuwa hatua za kurekebisha ufisadi wa asili wa Demokrasia. Tumekuwa kama watu tuliogandishwa, hatuwezi kusonga mbele kwa uongozi uliopo, wala kurudi nyuma kwenye uongozi uliopita. Katika hali hii, lazima tujiulize: kwani hakuna njia ya jeshi letu kutoa Nussrah yake kwa Hizb ut Tahrir kwa kurejesha tena Khilafah kwa njia ya Utume?




Bila shaka, Khilafah ni njia ya utawala katika Uislamu, kuchunga mambo yetu kwa mujibu na Qur’an na Sunnah, kiasi kwamba kila sheria na kifungu cha katiba yake ni kwa mujibu wa dalili ya wahyi. Zaidi ya hayo, Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) ameweka ufaradhi wa Bay’ah (ahadi ya utiifu) kwa Khalifah kwa kuufunga kwa kutokuwepo kwake na kifo kibaya zaidi kati ya vifo vyote, kufa kwa kisichokuwa Uislamu,

**«مَنْ مَاتَ وَلَيْسَ فِي عُنُقِهِ بَيْعَةٌ مَاتَ مِيتَةً جَاهِلِيَّةً» “Yeyote anayekufa bila kuwa na Bay’ah (ahadi ya utiifu) shingoni mwake amekufa kifo cha kijahiliya”** (Muslim). Ni faradhi juu ya kila mmoja wetu kuwa na Bay’ah kwa Khalifah iwepo katika kipindi chetu. Hakika, huu ni muda wa Khilafah.

**Musab Umair**

# Khilafah Ikavunjwa … kwa hiyo wanaoabudu ng'ombe nchini India wakawashinda nguvu "Ummah Bora Uliotolewa kwa Watu"… Enyi Majeshi ya Waislamu kwa Nini Hamuchangamki?!




Tangu Februari 24, 2020, mji mkuu wa India, Delhi, umekuwa ukishuhudia mauaji yanayotekelezwa na wanaoabudu ng'ombe dhidi ya Waislamu. Zaidi ya Waislamu 40 wameuawa na zaidi ya 200 wamejeruhiwa. Kwani ilikuwa ni adhabu kwa Waislamu kwa kuandamana dhidi ya utekelezwaji wa Sheria ya Mabadiliko ya Uraia ya 2019.

Ni wazi kwamba ushirikiano wa polisi na vikosi vya India pamoja na wahalifu ni dalili wazi ya chuki ya serikali ya India dhidi ya Waislamu, na wapambe wake walishuhudia mauaji na uchomaji wa kidhalimu uliotekelezwa na majangili wao dhidi ya Waislamu. Na hata kuwachochea kufanya hivyo. Mauaji ndani ya Delhi yalifanana na udhalimu wa Mauaji ya Gujarat yaliyotokea mnamo 2002 na kuua zaidi ya Waislamu 2,000.

Wapiga kura ndani ya Delhi, mji mkuu walipiga kura dhidi ya BJP, chama kilipoteza viti 64 kati ya 72, ikijumuisha kushindwa kwa chama cha Bharatiya Janata Mala Kapil Mishra kilichoandaa mauaji kama kulipiza kisasi kwa kushinwda kwake. Mauaji yaliyotokea baada ya ilani ya saa 24 iliyotoka kwa Kapil Mishra kwenda kwa polisi wa Delhi ili kuwashinda nguvu

waandamanaji wa sheria ya kiubaguzi na kueneza upotezaji uhai na uharibifu wa mali na misikiti.




Chuki dhidi ya Waislamu imekuwa ndio kilele cha dhamana ya magaidi Wahindu, ambao walikuwa makini kusambaza video zilizorekodiwa wakati wakitekeleza uhalifu wao pasi na hofu ya kuhesabiwa na sheria. Na hata polisi wakisimama bega kwa bega na magaidi Wahindu, pia wamekuwa wakionekana wakirekodi video za mauaji. Hii inaweka wazi muda wa utekelezaji wa mauaji haya ili kusadifiana na ziara ya Rais wa Amerika Trump ikijumuisha kauli ya Trump ya kutojali hali ya Waislamu nchini India na kutojali kwa Amerika kuhusiana na kuteswa kwa Waislamu, katika hotuba iliyotolewa mnamo Februari 24, 2020 katika Uwanja wa Motera ndani ya Ahmedabad. Trump alionyesha ni kiwango gani Amerika na India zinachukia Uislamu na Waislamu pale alipoweka wazi nia yake ya kuendelea na vita dhidhi ya kile alichokiita ‘Msimamo Mkali wa Kiislamu’ kwa kushirikiana na India na kuashiria Amerika kuishinda Dola ya Kiislamu. Msimamo wa Trump ulikuwa sambamba na mradi wa Amerika, ulioifanya India ni eneo lenye nguvu ya kuidhibiti Uchina na kuweka kikwazo dhidi ya kusimamishwa kwa Dola ya Khilafah.

**Enyi Waislamu**

Jueni ya kwamba demokrasia kubwa duniani imethibitisha kila mara kwamba nidhamu ya Kikafiri ya kidemokrasia haiwezi kuongoza nchi yao. Demokrasia inaruhusu wanaoiamini kuvuka mipaka ili kufaulisha maslahi ya warasilimali na kuwafurahisha wengi ili kuhakikisha kwamba wanaingia uongozini. Ilhali nidhamu ya utawala ya Uislamu, Khilafah, inasimama katika mipaka ya Mwenyezi Mungu (swt) na iko kwa ajili ya ustawi wa watu na sio kuridhisha na kufurahisha tabaka lolote na kulitenga jingine ndani ya jamii kwa hali yoyote ile itakavyotekelezwa.

**Enyi Waislamu wa India**




Jueni ya kwamba Mwenyezi Mungu (swt) amezifunga Ajal na Rizq (uhai na riziki) zenu. Na Yeye (swt) ndiye Mbora wa Kutoa Riziki. Na Yeye (swt) amebadilishana na Waumini uhai wao na mali zao kwa Jannah. Hizi ni zama za mitihani ambapo munatakiwa kusimama kwa pamoja na kuwakabili Makafiri na Washirikina. Musitafute salama ndani ya usekula na demokrasia, kwa sababu pamoja na kuwa ni nidhamu ya kikafiri, imefeli na yeyote anayeifuata atakuwa ni katika waliofeli. Vilevile, utaifa haujawaletea manufaa yoyote. Bali mulichovuna ni chuki na ubaguzi kutokana nao. Mauaji na mauaji munayopitia kupitia mikono ya Wahindu ni ushahidi tosha kwa yale tunayo yasema.

Jukumu la kudumisha usalama wenu upo kwa serikali. Hata hivyo, serikali inapozembea katika kutekeleza wajibu wake basi wao wenyewe ndio wanaoshiriki kwa njia ya moja kwa moja au isiyokuwa ya moja kwa moja katika kuwaua na kuwadhuru nyinyi. Kwa hiyo, ni wajibu kwa Waislamu kulinda roho, mali na heshima yao kwa njia yoyote ile. Ni wajibu kwa mujibu wa Shari’ah. Nabii wa Mwenyezi Mungu (saw) alisema: « مَنْ قُتِلَ دُونَ مَالِهِ فَهُوَ شَهِيدٌ وَمَنْ قُتِلَ دُونَ أَهْلِهِ أَوْ دُونَ دَمِهِ أَوْ دُونَ دِينِهِ فَهُوَ شَهِيدٌ» **“Yeyote atakayeuawa akiwa anatetea mali yake, ni shahidi. Yeyote atakayeuawa akiwa anailinda familia yake, ni shahidi. Yeyote atakayeuawa akiwa anailinda dini yake, ni shahidi. Yeyote atakayeuawa akiwa anajilinda mwenyewe, ni shahidi.”** (Sunan Abu Dawood)




**Enyi Majeshi nchini Pakistan, Bangladesh na nchi nyingine za Waislamu:**

Damu haikuchemka katika mishipa yenu pale mulipowaona wanaoabudu ng’ombe na masanamu wakiwadhuru kaka na dada zenu Waislamu na kukiuka heshima yao ilhali mumefungwa ndani ya kambi zenu mipakani, je Delhi na Lahore hazimo ndani ya Pakistan katika eneo la Punjab haswa?! Kwani hamusomi maneno ya Mwenyezi Mungu (swt), [ وَإِنِ اسْتَنْصَرُوكُمْ فِي الدِّينِ فَعَلَيْكُمُ النَّصْرُ] **“Lakini wakiomba msaada kwenu katika Dini, basi ni juu yenu kuwasaidia.” Kwani munawaheshimu watawala wanaodhuru na kukubali migawanyiko ya Uingereza ndani ya Waislamu na hamuitikii maneno ya Nabii wa Mwenyezi Mungu (saw)?**

Nabii wa Mwenyezi Mungu (saw) alisema: « الْمُسْلِمُونَ تَتَكَافَأُ دِمَاؤُهُمْ يَسْعَى بِذِمَّتِهِمْ أَدْنَاهُمْ وَيُجِيرُ عَلَيْهِمْ أَقْصَاهُمْ وَهُمْ يَدٌ عَلَى مَنْ سِوَاهُمْ يَرُدُّ مُشِدُّهُمْ عَلَى مُضْعِفِهِمْ وَمُتَسَرِّيهِمْ عَلَى قَاعِدِهِمْ لَا يُقْتَلُ مُؤْمِنٌ بِكَافِرٍ وَلَا ذُو عَهْدٍ فِي عَهْدِهِ» **"Waislamu wako sawa ukizingatia damu. Wachini katika wao anastahiki ulinzi kwa niaba yao, na anayeishi mbali anaweza kutoa ulinzi kwa niaba yao. Ni sawa na mkono mmoja dhidi ya wote walioko nje ya jamii. Wale walio na vipando vya haraka wawarudie walio na vipando vya polepole, na wale waliotoka nje na kikundi (lazima warudi) kwa wale walioko kituoni. Muumini hatouawa kwa ajili ya kafiri, wala mshirika wake aliyeko katika ushirika naye."** (Sunan Abu Dawud).

Khilafah Rashidah kwa njia Utume, itakayosimamishwa hivi karibuni, kwa idhini ya Mwenyezi Mungu, itaihesabu Amerika na India na yeyote yule aliyefanya uhalifu dhidi ya Uislamu na Waislamu, na adhabu ya Akhera ni kubwa zaidi lau wangelikuwa wanafahamu!

[[إِنَّ بَطْشَ رَبِّكَ لَشَدِيدٌ]] **"Hakika kutesa kwa Mola wako Mlezi ni kukali."** [Al-Buruj: 12]


**Salah Eddine Adada**

## Ni Miaka Tangu Kuanguka kwa Khilafah... Mpaka Lini Tutaendelea Kubakia kama Mayatima Katika Meza za Mabwana Walafi?! (Imetafsiriwa)



**Enyi Waislamu:**

Katika siku hii, 03/03/1924 M sawia na 28 Rajab 1342 H, wasaliti katika Waarabu na Waturuki wakishirikiana na makafiri wa kikoloni wakiongozwa na Uingereza kwa wakati huo, na kuiangusha dola ya Khilafah, dola ambayo iliwaunganisha na kuwalinda Waislamu. Na kutokana na kuanguka huko dunia ilitikisika chini ya miguu yao na ardhi yao ikawa chini ya ushawishi mkoloni Kafiri na kuikatakata vipande, na kupachika msaliti katika kila kipande cha ardhi kama mtawala (wakimuamrisha naye akifuata, na wakimkataza naye akiacha), na waliwaorodhesha kufanya kila aina ya jambo bila kujali ni baya kiasi gani , ili kuzuia kurejea tena kwa Uislamu na Khilafah, hivyo basi watawala walioko wamekuwa mstari wa mbele kutekeleza sera hatari dhidi ya Uislamu na Waislamu kwa ujumla.



VOL. XXXIII. NO. 55 BRIDGEPORT, CONN., TUESDAY MO

CALIPHATE ABOLISHED BY TURKEY

Caliph Abdul Medjid Deposed By Angora Assembly, Terminating Religious Reign Over Moslem World.

BRITAIN UNEASY BECAUSE OF INDIA

Effect of Turkish Government's Drastic Act May Reverber-

Undertakers To Remove Gloom From Trappings

WAYS AND MEANS COMMITTEE HEARS

B. H. S. ASSEMBLY HALL CROWDED AS WEIZMAN SPEAKS

Over 10,000 Pledged Spontaneously as Palestine Foundation Fund Drive Is Opened In City.

POLISH PARLIAMENT MEMBER IS PRESENT

Master Chemist and Chief Rabbi of Seacow, Poland, Are Honored Guests of Bridgeport.

Resignation of F Constable May As Result of I

Tangu siku hiyo ya huzuni, majanga na mashaka yametufunika sisi Waislamu, mauaji yametuzunguka kushoto, kulia na katikati. Mayahudi, waliokuwa wamekwama katika udhalili, wamewezeshwa na Uingereza kuivamia ardhi ya Palestina - ardhi ya Israa na Mi'raj, na kuimarishwa na Amerika, ambayo imekusanya mataifa kwa ajili ya kupambana na Uislamu na Khilafah, kwa hiyo wakaiharibu Iraq na Afghanistan, na rais wake, Trump, ametembelea India, baada ya muda Wahindu wakaanza kuwadhalilisha na kuwaua Waislamu… ilhali nchini Uchina, Ummah wote umetiwa jela kwa kuwa ni Waislamu. Ama katika nchi ambazo Waislamu wanaandamana kupinga nidhamu ya Kimagharibi na vibaraka wake, mataifa ya kiulimwengu yakaungana dhidi yao kumsaidia mchinjaji wa Ash-Sham katika kuwachinja Waislamu kila siku, na wanaingiliakati nchini Yemen na Libya, na kuziingiza katika vita visivyoisha na kuwapasua.

Ama kuhusu Tunisia, ambayo ilikuwa ndio nukta kianzio cha mapinduzi, wajumbe wa kikoloni, mashirika ya kimataifa na mashirika yasiyo ya kimataifa yalifurika nchini ili kuzuia kuanguka kwa mfumo wa kisekula wa kirasilimali, na Tunisia kubakia masikini, iliyotengwa na kuwa ni mali ya Wamagharibi. Wamelazimisha katiba za kisekula, na kuwatumia vibaraka wao, kudhibiti vyeo muhimu na idara katika dola na tumebakia kudhalilishwa kiasi kwamba balozi wa Uingereza ndiye anayeamua nani awe Rais, na serikali yote, na kuweka sera zake, na IMF inaamua mipango yake ya kiuchumi…

**Enyi Waislamu katika Ardhi ya Zaytuna:**

Hii ndio dola na hali ya Waislamu leo; mpasuko, mgawanyiko, ukoloni na udhalilishaji. Takribani miaka miaka mia moja, Ummah umeishi bila dola, bila Khilafah, wala Khalifah, tunaishi kama Waislamu, na ilhali Uislamu umewekwa mbali na uongozi, siasa, uchumi na nidhamu nyingine za maisha. Kwa hiyo, imepelekea uharibifu na ufisadi kuwa juu katika ardhi zetu, na mkoloni Kafiri kutuongoza, na vibaraka kuwa juu yetu mpaka tumekosa fahari na hadhi, kiasi kwamba Muislamu anadhalilishwa popote aendapo. Sababu iko wazi, tumeambiwa na Al-Faruq (ra), alisema: **“Tulidhalilishwa na Mwenyezi Mungu akatupa hadhi kupitia Uislamu, kwa hiyo lau tutatafuta utukufu kupitia chochote kile kisichokuwa Uislamu, basi Mwenyezi Mungu atatudhalilisha.”**




**Enyi Waislamu katika Ardhi ya Zaytuna, Ardhi ya Wakombozi Mashujaa,**

**Mwenyezi Mungu** (swt) anasema

[قِينَ لَا يَعْلَمُونَ وَلِلَّهِ الْعِزَّةُ وَلِرَسُولِهِ وَلِلْمُؤْمِنِينَ وَلَٰكِنَّ الْمُنَاف ...]

**“… Na Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye utukufu – Yeye, na Mtume wake, na Waumini. Lakini wanafiki hawajui.”** [Al-Munafiqun: 8]

Ukoloni haukuandikiwa kudumu, ila tatizo ni ukimya wetu kuhusu ukoloni na vibaraka wake katika ardhi zetu. Tunawakukumbusha katika siku hii ya maumivu ya kukumbuka kuangushwa kwa Khilafah, dola ambayo ilifanyakazi ya kutuunganisha sisi pamoja na Waislamu wengine. Wakati huo, Tunisia ndio ilikuwa ndio kiongozi upande wa magharibi wa Khilafah kwa karne nyingi, na ilikuwa ndio kiongozi katika ukanda wa Mediterranean, na wakati Khilafah ilivunjwa ilhali tuko kimya, na Uislamu ukaondoshwa ilhali tumeridhia, na ardhi zetu zikawa duni vijipande!




Leo hii, ilhali mapinduzi yamechipuka katika nchi yenu ambayo yametikisa ardhi za nchi za kikoloni, (kwa sababu ni mapinduzi ya Ummah ambayo yamesambaa katika ardhi zote za Waislamu, na kuashiria kuanguka kwa tawala zao, kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu). Tunawahutubia ili kuwakumbusha utukufu ambao ulijengwa na mababu zenu, na tunaweza kuurudisha tena leo kwa sababu Uislamu uliowapandisha daraja mababu zetu bado upo baina yetu kama ulivyoteremshwa kwa Mtume wetu (saw), na miongoni mwenu kunao viongozi wenye akili na utambuzi: Hizb ut Tahrir; kiongozi asiyedanganya. Na munaifahamu vizuri kwa ukweli wa maneno na vitendo vyake, ikiwa haitafuti zawadi wala sifa kutoka kwa yeyote, isipokuwa ikitafuta radhi za Mwenyezi Mungu (swt) kwa kutekeleza shari’ah Zake ardhini, kwa kuitikia mwito wa Mwenyezi Mungu (swt)

[ فَلَا وَرَبِّكَ لا يُؤْمِنُونَ حَتَّى يُحَكِّمُوكَ فِيمَا شَجَرَ بَيْنَهُمْ ثُمَّ لا يَجِدُوا فِي أَنْفُسِهِمْ حَرَجاً مِمَّا قَضَيْتَ وَيُسَلِّمُوا تَسْلِيماً]

**“La! Naapa kwa Mola wako Mlezi! Hawataamini mpaka wakufanye wewe ndiye muamuzi katika yale wanayo khitalifiana, kisha wasione uzito katika nyoyo zao juu ya hukumu utakayotoa, na wanyenyekee kabisa.”** [An-Nisa: 65].

Hivyo basi, muonyesheni Mwenyezi Mungu (swt) yaliyo mazuri, na ondosheni dhambi ya kutelekeza mwito wa Bwana wenu. Kama Waislamu hatusamehewi mpaka tufanye kazi kwa bidii ya kusimamisha taji lililipotea la wajibu (taj al-fard); Khilafah ya Uongofu kwa njia ya Utume, ambayo kwa uhakika inatarajiwa hivi karibuni. Ni ahadi ya Mwenyezi Mungu (swt): Ambaye alisema:




**[ وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْناً يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئاً...]**

**“**Mwenyezi Mungu amewaahidi wale walio amini miongoni mwenu na wakatenda mema, ya kwamba atawafanya makhalifa katika ardhi kama alivyo wafanya makhalifa wa kabla yao, na kwa yakini atawasimamishia Dini yao aliyo wapendelea, na atawabadilishia amani baada ya khofu yao. Wawe wananiabudu Mimi, wala wasinishirikishe na chochote. Na watao kufuru baada ya hayo, basi hao ndio wapotovu.**...”** [An-Nur: 55]

# Picha za Kampeni

Wanaharakati wa Hizb ut-tahrir Kenya wakitekeleza maandamano baridi sehemu tofauti tofauti kuwakumbusha ummah juu ya kuvunjwa kwa Khilafah ndani ya mwezi wa Rajab, 1342



Amali za Kiulimwengu za Hizb ut Tahrir

Katika Kukumbuka
Kuanguka kwa Khilafah 99

1441H - 2020M